Tuzo ya Hadithi Fupi ya Jumuiya ya Madola 2019

Sifa Stahiki na Masharti ya Kushiriki

Tafadhali soma sifa stahiki na masharti ya kushiriki kabla ya kuanza mchakato wa kujaza fomu mtandaoni. Fomu ya mtandaoni inapatikana kuanzia siku ya ufunguzi: tarehe 1 Septemba, 2018.

Unapowasilisha hadithi inahesabiwa kuwa umekubali masharti ya kushiriki.

Iwapo una maswali yoyote kuhusu sifa stahiki na masharti ya kushiriki ambayo hayajajibiwa hapo chini, tafadhali tuma barua pepe writers@commonwealth.int kwa ajili ya ufafanuzi kabla ya kuwasilisha hadithi yako.

Siku ya Ufunguzi

1 Septemba 2018

Tarehe ya mwisho

Tarehe ya mwisho ya kupokea fomu ya kushikiri mtandaoni ni tarehe 1 Novemba 2018 (Saa 5.59 usiku katika kanda muda yoyote)

Hadithi zinazowasilishwa baada ya tarehe hiyo hazitafikiriwa.

1. **Kuhusu Tuzo**

a. Tuzo ya Hadithi Fupi ya Jumuiya ya Madola ni tuzo ya kila mwaka kwa ajili ya hadithi fupi ambazo hazijawahi kuchapishwa, tuzo ambayo husimamiwa na kugharamiwa na Commonwealth Foundation.

b. Tuzo ya Hadithi Fupi ya Jumuiya ya Madola huendeshwa na Waandishi wa Jumuiya ya Madola, mradi wa utamaduni wa Commonwealth Foundation.

c. Tuzo inafikia kanda tano za Jumuiya ya Madola ambazo ni 1. Afrika, 2. Asia, 3. Kanada na Ulaya, 4. Bahari ya Karibi na 5. Bahari ya Pasifiki (Ona Sehemu 4 kwa nchi katika kila kanda)

d. Jopo la majaji la kimataifa lina jaji moja kutoka kwa kila kanda. Tafadhili elewa kwamba, ingawa hadithi zote zitaamuliwa kikanda, majaji wote watasoma na kutafakari juu ya hadithi zinazotoka kila kanda.

e. Kutakuwa na washindi watano, mmoja kutoka kila kanda. Kati ya washindi kikanda, mmoja atateuliwa kama mshindi mkuu. Mshindi mkuu wa Tuzo ya Hadithi Fupi ya Jumuiya ya Madola atapokea £5,000 na washindi wengine wanne wa kana watapokea £2,500. Iwapo hadihi inayoshinda imetafsiriwa Kiingereza, mtafsiri naye atapokea pesa za tuzo za ziada.

f. Uteuzi wa mwisho wa hadithi utafanywa na jopo la kimataifa la majaji; wasomaji wenye uzoefu watawasaidia majaji hao katika kuteua orodha ya awali ya hadithi.

2. **Sifa Stahiki**

a. Lazima washiriki wawe raia wa nchi ya Jumuiya ya Madola – tafadhali ona Sehemu ya 4 kwa orodha ya nchi za Jumuiya ya Madola. Commonwealth Foundation itaomba kupata uthibitisho wa uraia kabla ya kuwateua washindi. Waandishi kutoka kwa nchi nyingine ambazo hazimo kwenye Jumuiya ya Madola hawana sifa stahiki.

b. Kwa sababu za kikanda, hadithi zitapangwa kulingana na nchi ya uraia ya mwandishi. Mwandishi akiwa na raia pacha, uraia wake utachukuliwa kulingana kwa mujibu wa makazi yake ya kudumu.

c. Si lazima mwandishi awe anaishi kwa sasa kwenye nchi ya Jumuiya ya Madola, ili mradi ni raia wa nchi moja ya Jumuiya ya Madola.

d. Washiriki lazima wawe na umri wa miaka 18 au zaidi siku ya **tarehe 1 Novemba 2018**.

e. Commonwealth Foundation itakuwa na uamuzi wa mwisho kuhusu sifa stahiki, ikishauriana na mwenyekiti katika kufanya maamuzi. Maamuzi ya mwenyekiti kuhusu suala la sifa stahiki ni ya mwisho na hakuna nafasi ya kuwasiliana zaidi juu ya hilo..

f. Washindi wakuu wa Tuzo ya Hadithi Fupi ya Jumuiya ya Madola huko nyuma hawaruhusiwi kushiriki tena. Washindi wa kanda huko nyuma wanaruhusiwa.

g. Wafanyakazi wa sasa wa Commonwealth Foundation hawaruhusiwi kushiriki.

h. Hadithi zisiwe zimechapishwa na zisichapishe katika lugha yoyote kabla ya Mei 1 2019.

3. Masharti ya ushiriki

a. Hadithi, pamoja na zinazotafsiriwa lazima ziwasilishwe na mwandishi mwenyewe.

b. Hadithi zitakubaliwa ikiwa tu zimewasilishwa kupitia kwa fomu ya mtandaoni.

c. Siku ya mwisho ya kupokea hadithi ni tarehe 1 Novemba 2018 (Saa 5.59 usiku katika kanda muda yoyote).

d. Mwandishi anaruhusiwa kuwasilisha hadithi moja tu kwa ajili ya Tuzo ya Hadithi Fupi ya Jumuiya ya Madola.

e. Hadithi lazima iwe ya mwandishi mwenyewe anayewasilisha.

f. Hadithi lazima iwe mpya kabisa na isiwe imechapishwa mahali popote, iwe ni hadithi nzima au sehemu yake **katika lugha yoyote** kabla ya **tarehe 1 Mei, 2019**. Kuchapishwa maana yake ni kutolewa katika namna yoyote inayofikika na watu, k.m. mkusanyiko, jarida, gazeti. Aidha maana yake ni kuchapisha mtandaoni isipokuwa kwenye blogu na tovuti binafsi.

g. Hadithi zilizowasilishwa katika Tuzo ya Hadithi Fupi ya Jumuiya ya Madola huko nyuma hazikubaliki.

h. Hadithi ziwasilishwe kwa lugha ya kiingereza, isipokuwa lugha zifuatazo: raia wa Jumuiya ya Madola wanaoandika kwa lugha ya Kibengali, Kichina, Kiswahili, Kimalay, Kireno, Kisamoa, Kitamil, ambao hawana tafsiri ya hadithi zao katika Kiingereza, wanaruhusiwa kuwasilisha hadithi zao katika lugha yao ya asili. Hadithi fupi zingine ambazo zimetafsiriwa katika Kiingereza zina sifa stahiki pia ili mradi hadithi inawasilishwa na mwandishi (siyo mtafsiri), na ili mradi kwamba mtafsiri naye ni raia wa nchi ya Jumuiya ya Madola. .

i. Mwandishi anaruhusiwa kuwasilisha hadithi kwenye tuzo zingine pia, ili mradi mwandishi anatoa taarifa kwa Tuzo mara moja iwapo hadithi yake inakubalika kuchapishwa kwingine au kuteuliwa kupata tuzo.

j. Hadithi zisiwe chini na maneno 2,000 na zisizidi maneno 5,000 (pamoja na kichwa cha hadithi).

k. Hadithi ziwasilishwe kwenye PDF. Tafadhali hifadhi hadithi kama PDF na tumia kichwa kwa hadithi kama jina la faili. Tafadhili zingatia kwamba hadithi haitakiwi kuhifadhiwa kama "Hadithi ya Jumuiya ya Madola" au kichwa chochote kingine. Iwapo huwezi kuhifadhi kama PDF, unaweza kutuma kwenye Microsoft Word kwa jina kama iliyvoelezwa hapo juu. Ukurasa wa kwanza uwe na jina la hadithi na idadi ya maneno.

l. Maelezo juu ya mwandishi uwekwe kwenye fomu ya kushiriki. Yasioneshwe mahali popote pengine. Hadithi zote zinaamuliwa bila kujua jina la mwandishi..

m. Panapotakiwa, maelezo juu ya tafsiri yawepo pia kwenye fomu ya kushiriki..

n. Hadithi zote ziwasilishwe katika herufi ya ukbuwa wa pointi 12 ya font ya Arial na kuacha nafasi mbili baina ya mistari. Kurasa zote ziwe na namba na kichwa chenye jina la hadithi..

o. Mwandishi yuko huru kuchagua mandhari, mtindo na dhamira ya hadithi

p. Hadithi iwe inawalenga watu wazima. Isiwe imeandikiwa kwa ajili ya watoto tu.

q. Washiriki wanakubali, kama sharti ya kushiriki, kwamba waendeshaji wanaweza kutangaza kwamba hadithi imewasilishwa au kuteuliwa katika orodha ya kuamuliwa kupata Tuzo.

r. Hakimiliki ya kila hadithi inabaki kuwa ni mali ya mwandishi kote duniani. Waandishi wa Jumuiya ya Madola watakuwa na haki bila kizuizi ya kuchapisha hadithi zilizoshinda (mshindi mkuu na mshindi kikanda) katika mkusanyiko na kwa ajili ya kutangaza.

s. Mshindi mkuu na washindi wa kanda watategemewa kushiriki katika shughuli za kujitangaza, zikiwemo katika mitandao ya jamii panapowezekana.

t. Mshindi mkuu na washindi wa kanda watategemewa kushiriki katika programu iliyopangwa na kukubaliwa nao ya kuwafikia kanda ili kuendeleza na kutangaza Waandishi wa Jumuiya ya Madola.

4. Kanda za tuzo

Africa: Botswana, Cameroon, eSwatini, The Gambia, Ghana, Kenya, Lesotho, Malawi, Mauritius, Mozambique, Namibia, Nigeria, Rwanda, Seychelles, Sierra Leone, South Africa, Tanzania, Uganda, Zambia. Overseas Territories: Saint Helena, Tristan Da Cunha, Ascension Island.

Asia: Bangladesh, Brunei Darussalam, India, Malaysia, Pakistan, Singapore, Sri Lanka.

Canada and Europe: Canada, Cyprus, Malta, United Kingdom. Overseas Territories: Gibraltar, Falkland Islands.

Caribbean : Antigua and Barbuda, Bahamas, Barbados, Belize, Dominica, Grenada, Guyana, Jamaica, Saint Kitts and Nevis, Saint Lucia, Saint Vincent and the Grenadines, Trinidad and Tobago. Overseas Territories: Anguilla, Bermuda, British Virgin Islands, Cayman Islands, Montserrat, Turks and Caicos Islands.

Pacific: Australia, Fiji, Kiribati, Nauru, New Zealand, Papua New Guinea, Samoa, Solomon Islands, Tonga, Tuvalu, Vanuatu. Overseas Territory: Pitcairn.